BARAZA LA WAWAKILISHI ZANZIBAR

Simu Nam. + 255 24 2230602/1
Fax Nam. + 255 24 2230215
Tovuti: www.zanzibarassembly.go.tz

SANDUKU LA BARUA 902,
ZANZIBAR
Barua Pepe: zahore@zanlink.com

# HOTUBA YA MAONI YA KAMATI YA USTAWI WA JAMII KUHUSU MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI YA WIZARA YA AFYA KWA MWAKA WA FEDHA 2023/2024

**Mheshimiwa Spika,**
Awali ya yote tunamshukuru Allah (S.W.T) mwingi wa rehma na utukufu, kwa kutujaalia uhai na afya njema, na kutuwezesha kukutana tena katika Baraza hili la kumi, kwa dhamira ya kuendelea kuwatumikia wananchi wa Zanzibar ambao ndio sababu ya sisi kusimama katika Baraza hili.

**Mheshimiwa Spika,**
Aidha, nakushukuru na kukupongeza wewe Mheshimiwa Spika, kwa jitihada zako na namna unavyoliongoza Baraza hili tukufu kwa ustadi mkubwa. Ni imani yetu kwamba, utaendelea kutuongoza kwa uadilifu na ufanisi wa hali ya juu kwa lengo la kuimarisha Demokrasia katika chombo hiki muhimu.

**Mheshimiwa Spika,**
Vile vile, nichukue fursa hii adhimu kumpongeza Mhe. Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Dkt. Hussein Ali Hassan Mwinyi kwa kazi nzuri na kubwa ya kutuletea maendeleo nchini. Vile vile, tunawapongeza wasaidizi wake Makamu wa Kwanza wa Rais Mhe. Othman Masoud Othman na Makamu wa Pili wa Rais Mhe. Hemed Suleiman Abdulla kwa kumsaidia vyema Mhe. Rais wetu katika kutekeleza majukumu yake.

**Mheshimiwa Spika,**
Pia, naomba kuchukua fursa hii, kumshukuru na kumpongeza kwa dhati Mhe. Waziri, Mhe. Naibu Waziri, Katibu Mkuu pamoja na Watendaji wake wote kwa jitihada kubwa wanazozichukua katika kulipeleka mbele gurudumu la maendeleo ya nchi yetu.

**Mheshimiwa Spika,**
Kwa namna ya pekee, nawashukuru Wajumbe wote wa Kamati ya Ustawi wa Jamii kwa kazi kubwa na nzuri wanazozifanya wakati wote wa kazi za Kamati, jambo ambalo limepelekea wepesi kwangu kuweza kuiongoza Kamati hii inayosimamia Wizara muhimu kabisa. Wajumbe wa Kamati wameonesha umahiri, weledi na umakini wa hali ya juu na wameweza kuijadili ipasavyo Bajeti hii na kuhoji mambo mengi ya msingi, kwa lengo la kuhakikisha fedha wanazoidhinisha katika Baraza hili, zinatumika vizuri na kwa lengo la kuwaletea maendeleo wananchi wa Zanzibar.

**Mheshimiwa Spika,**
Napenda kutumia fursa hii pia, kuwapongeza na kuwashukuru Wawakilishi wote waliomo katika Baraza lako Tukufu, kwa kuendelea kuwawakilisha na kuwatumikia wananchi na makundi yaliowachagua. Ni wazi kwamba wananchi wamejenga imani kubwa kwetu, nasi hatuna budi kurejesha imani kwao, kwa kuwatumikia kwa dhati na kwa moyo wetu wote, kwa dhamira ya kutetea maslahi yao katika Baraza hili tukufu.

**Mheshimiwa Spika,**
Kabla ya kuendelea na hotuba hii, kwa ruhusa yako, na kwa heshima ya kipekee naomba niwatambue Wajumbe wa Kamati ya Ustawi wa Jamii kama ifuatavyo:-

| | | |
|---|---|---|
| 1. Mheshimiwa Mohamed Ahmada Salum | - | Mwenyekiti |
| 2. Mheshimiwa Mwantatu Mbarak Khamis | - | M/Mwenyekiti |
| 3. Mheshimiwa Abdalla Abasi Wadi | - | Mjumbe |
| 4. Mheshimiwa Bihindi Hamad Khamis | - | Mjumbe |
| 5. Mheshimiwa Haji Omar Kheri | - | Mjumbe |
| 6. Mheshimiwa Zawadi Amur Nassor | - | Mjumbe |

**Mheshimiwa Spika,**
Aidha, Kamati hii inafanyakazi kwa kusaidiwa na Makatibu wawili ambao wamekuwa wakitusaidia kwa kiasi kikubwa na kwa uweledi wa hali ya juu katika kutekeleza majukumu yetu, msaada wa makatibu hao umekuwa chachu ya mafanikio makubwa ya Kamati hii. Makatibu hao na Msaidizi ni:

| | |
|---|---|
| 1. Ndg. Fatma Omar Ali | Katibu |
| 2. Ndg. Mussa Issa Mussa | Katibu |
| 3. Ndg. Azmina Hamad Khamis | Msaidizi |

**Mheshimiwa Spika,**
Moja kati ya jukumu la msingi la Kamati yetu ni kuchambua mapendekezo ya Serikali, kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya kila mwaka, hivyo katika kutekeleza jukumu hilo Kamati yangu ilikaa na kuijadili na hatimaye kupitisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Afya, sasa kwa ruhusa yako na kwa niaba ya Kamati, napenda kuwasilisha Maoni ya Kamati kuhusiana na Bajeti hiyo kwa mwaka wa fedha **2023/2024.**

**Mheshimiwa Spika,**
Baada ya utangulizi huo, sasa naomba nitekeleze jukumu nililopewa na Kamati la kuwasilisha Maoni ya Kamati, mbele ya Baraza lako tukufu.

**Mheshimiwa Spika,**
Wizara ya Afya kwa mwaka wa fedha **2023/2024** ina Mafungu (votes) **mbili (2)** ambapo **Fungu H01 Wizara ya Afya** na limepanga kutekeleza Programu Kuu Tatu (3) zenye Programu Ndogo Saba **(7)** na **Fungu HO2 Hospitali ya Mnazi Mmoja** na imepanga kutekeleza Programu Kuu Mbili (2) zenye Programu Ndogo Tatu (3) na ambapo kwa ujumla fedha zilizoombwa kwa Wizara ya Afya ni **TZS. 189,379,436,000/= (Bilioni Mia Thamanini na Tisa, Milioni Mia Tatu na Sabiini na Tisa, Laki Nne na Thelathini na Sita)** na kwa Hospitali ya Mnazi Mmoja zimeombwa jumla ya **TZS. 1,348,585,000/= (Bilioni Moja, Milioni Mia Tatu na Arubaini na Nane, Laki Tano na Thamanini na Tano).**

## FUNGU H01 WIZARA YA AFYA
## PROGRAMU KUU YA HUDUMA ZA TIBA

**Mheshimiwa Spika,**
Programu Kuu hii inatekelezwa kupitia Programu Ndogo mbili (2), ambazo ni **Programu Ndogo ya Huduma za Matibabu (SH010201)** na **Programu Ndogo ya Huduma za Uchunguzi (SH01020102)** inayohusiana na Huduma za Hospitali za Vijiji, Wilaya, Mkoa na Hospitali za Rufaa.

**Mheshimiwa Spika,**
Kamati, inachukua nafasi hii kuishukuru na kuipongeza Serikali ya Jamhuri ya Tanzania chini ya uongozi wa Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan pamoja na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar chini ya uongozi wa Mhe. Dkt. Hussein Ali Hassan Mwinyi kwa kuzielekeza fedha za Ahueni ya Uviko 19 kwa ajili ya ujenzi wa Hospitali za Wilaya kumi (10) na Hospitali ya Mkoa moja (1) kwa Unguja na Pemba.

**Mheshimiwa Spika,**
Lengo la ujenzi wa hospitali hiyo ni kuondoa msongamono wa wagonjwa wanaofika kwenye vituo vya afya na Hospitali za Wilaya pamoja na Hospitali ya Rufaa ili ziweze kutoa huduma bora kwa wagonjwa au wananchi wanaofika sehemu hizo.

**Mheshimiwa Spika,**
Pamoja na pongezi hizo, Kamati ilipata fursa ya kufanya ziara ya ukaguzi wa Miradi ya Ujenzi wa Hospitali zote za Wilaya na Mkoa kwa Unguja na Pemba zilizojengwa kwa fedha za Ahueni ya UVIKO 19 na kuweza kubaini baadhi ya mapungufu katika miradi hiyo ikiwemo Hospitali zote za Wilaya kukosa Mshauri Mwelekezi wa Mradi, hali hiyo imepelekea miradi kuchelewa kukamilika kwa wakati na kusababisha ongezeko la gharama za ujenzi wa miradi hiyo kufikia shilingi Bilioni 21.

**Mheshimiwa Spika,**
Vile vile, Kamati katika ziara waliyoifanya kwenye miradi hiyo kwa Unguja na Pemba imegundua kwa baadhi ya Hospitali za Wilaya zinazojengwa pamoja na zilizoanza kufanya kazi ya kutoa huduma za afya kuwepo kwa changamoto ikiwemo uvujaji mapaa, kutokuwepo kwa miundombinu imara ya maji, kutoanza kazi kwa mifumo ya TEHAMA, viyoyozi kutokufanya kazi, kuchelewa kwa vifaa kutoka kwa wasambazaji waliopewa kazi hiyo, ukosefu wa vifaa kama vile X-Ray mashine, pia vifaa vya kudhibiti umeme (*stabilizer*) baadhi ya majengo, hali inayopelekea hospitali hizo kushindwa kutoa huduma stahiki kama azma na malengo ya kuanzishwa kwake.

**Mheshimiwa Spika,**
Kutokana na mapungufu yote hayo tuliyoyataja, Kamati inaishauri Serikali
Kupitia Wizara ya Afya katika suala la miradi mikubwa kuweka Mshauri Mwelekezi kwa ajili ya kuepusha matumizi yasiyo ya lazima na kuweza kukamilisha mradi kwa wakati na kiwango kinachotakiwa pamoja na kupata usimamizi na ufuatiliaji wa karibu. Aidha, Kamati inashauri kukiongezea uwezo na wahandisi Kitengo cha Ufundi cha Wizara.

**Mheshimiwa Spika,**
Kamati, inaipongeza Taasisi ya Kimataifa ya "D-Tree International" kwa kushirikiana na Serikali kuisaidia jamii katika kutoa huduma za mama wajawazito pamoja na watoto chini ya miaka mitano katika kuwasaidia kuwapa ushauri nasaha ikiwemo lishe bora, kuhudhuria kwenye vituo vya afya kwa ajili ya kupima ujauzito pamoja na kujifungulia hospitali na

kuweza kuokoa vifo vingi vya mama na watoto.

**Mheshimiwa Spika,**
Taasisi hii inatoa huduma kupitia Vijana wanaojitolea katika Shehia za Unguja na Pemba "Community Health Volunteers (CHV)". Lakini huu ni mradi ambao utamaliza muda sio mrefu. Kamati inaishauri Serikali kupitia Wizara ya Afya kuanza kujiandaa kuuendeleza Mradi huu kwa kutenga fedha za bajeti kila mwaka kidogo kidogo kabla wafadhili hawajaondoka na kuweza kuendelea kutoa huduma hizo ndani ya Shehia nyumba kwa nyumba.

## PROGRAMU KUU YA UENDESHAJI NA URATIBU WA WIZARA YA AFYA

**Mheshimiwa Spika,**
**Programu Kuu** hii **PH0103** inatekelezwa na Programu Ndogo Nne (4) ambapo Kamati itajikita zaidi kwenye Programu Ndogo mbili ambapo **Programu Ndogo ya Utawala na Uendeshaji** (**SH010301**) na **Programu Ndogo ya Huduma ya Uratibu wa Mipango, Sera na Tafiti za Wizara (SH010302**).

**Mheshimiwa Spika,**
Kamati inaipongeza tena Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar ya Awamu ya Nane inayoongozwa na Mhe. Dkt. Hussein Ali Hassan Mwinyi kwa kuanzisha Sheria ya Mfuko wa Huduma za Afya Zanzibar kwa lengo la kuimarisha utoaji wa huduma za afya kwa wananchi wa ngazi zote.

**Mheshimiwa Spika,**
Kamati, inaishauri Serikali kwa upande wa wafanyakazi kuruhusiwa kuendelea kutumia Bima ya NHIF na nyengine kwa hiari licha ya kuanzishwa kwa Sheria inayowataka wafanyakazi wote wa Serikali kuwa chini ya Mfuko wa Huduma za Afya ulioanzishwa hivi karibuni.

**Mheshimiwa Spika,**
Vile vile, Kamati inaiomba Serikali kwa kushirikiana na Wizara husika kuharakisha mchakato wa matumizi ya Mfuko huo kama Sheria inavyoelekeza ili kwenda sambamba na azma na malengo ya kuanzishwa kwake.

**Mheshimiwa Spika,**
Kwa upande wa utekelezaji wa Miradi ya Maendeleo, Kamati

haikufurahishwa na taarifa ya iliyopatiwa kuhusu uendelezaji wa Mradi wa Ujenzi wa Maabara ya Bio-Chemistry Binguni, mradi ambao ulianza tokea Awamu ya Saba kwa lengo la kuwaondolea usumbufu wananchi wanaogundulika na maradhi ya mripuko. Mradi ambao fedha zake zilizikuwa zinaidhinishwa na Baraza la Wawakilishi kupitia Fungu la Bajeti la Wizara ya Afya, lakini jambo la kushangaza hadi tunamaliza bajeti hii ya mwaka 2022/2023 mradi huo bado utekelezaji wake ni wa kusuasua na Kamati inapohoji kukosa majibu sahihi.

Hivyo, Kamati inaiomba Serikali kuupa kipaumbele ukamilishaji wa mradi huu wa Maabara ya Bio-Chemistry ili Serikali pamoja na wananchi kuondokana na usumbufu wa usafirishaji wa sampuli za vipimo vya maradhi mbali mbali nje ya Zanzibar, hali inayoisababishia Serikali kukosa mapato yatokanayo na vipimo hivyo.

**Mheshimiwa Spika,**
Vile vile, Kamati inashauri Wizara kuangalia umuhimu wa kutekeleza ipasavyo Ibara ya 184(d) ya Ilani ya Uchaguzi ya CCM ya 2025 kuhusiana na Hospitali ya Binguni, kwani Kamati katika kazi zake za kufuatilia haijaona muendelezo wa ujenzi wa hospitali hiyo ambayo imetajwa ndani ya Ilani.

**Mheshimiwa Spika,**
Kamati, inaishauri Serikali kupitia Wizara ya Nchi, Ofisi ya Rais, Fedha na Mipango kwa mwaka huu wa bajeti 2023/2024 mradi huu utengewe fedha zinazotokana na ujenzi wa majengo kupitia usimamizi wa Tume ya Mipango.

**Mheshimiwa Spika,**
Pamoja na maelezo hayo, Kamati inapendekeza tena kwa Wizara kusimamia vizuri mapato kwa Taasisi zote ambazo zinakusanya na ziko chini ya Wizara ya Afya kwa ajili ya kufikia malengo ya makusanyo ya mapato yaliyokadiriwa na Serikali kwa mwaka husika wa bajeti.

**Mheshimiwa Spika,**
Vile vile, Kamati inashauri Wizara kuandaa Mpango Mkakati wa Wizara ya Afya kuhusu masuala ya Manunuzi mara baada ya kupitishwa kwa bajeti ya Wizara na Baraza la Wawakilishi katika Mkutano wa Bajeti kwa kila mwaka husika kwa lengo la kuweza kutekeleza mipango yake kwa wakati na kwa mafanikio, kwani Kamati imebaini mapungufu mengi yaliyotokea yalitokana na kutokuwepo kwa Mpango wa Manunuzi wa Wizara.

**Mheshimiwa Spika,**
Licha ya mafanikio yaliopo katika Wizara ya Afya, Kamati inapendekeza kwa watendaji wa Wizara kufanya kazi kwa mashirikiano na kuweza kufikia malengo waliyopangwa ya kutoa huduma bora kwa wananchi kwa maendeleo endelevu ya Taifa letu.

**Mheshimiwa Spika,**
Kamati, katika kufanya kazi zake imegundua kuwepo kwa ukosefu wa elimu juu ya utumiaji wa vifaa vya kieletroniki katika kuendesha shughuli zao. Hivyo, Kamati inaishauri Wizara kuwapatia mafunzo watendaji pamoja na madaktari waliopo katika hospitali zetu zilizojengwa ili kuondosha uharibifu wa mara kwa mara kwa mashine pamoja na matumizi ya vifaa kinyume na utaratibu.

**Mheshimiwa Spika,**
Kamati, inapendekeza kwa Serikali kupitia Wizara ya Afya kwa wataalamu wa afya wakiwemo madaktari, wauguzi na wakunga pamoja na wengine lazima wawe na leseni kabla ya kuanza kutekeleza majukumu yao ya kazi ili kuepusha matatizo mbali mbali ikiwemo kufanya kazi bila ya kuwa na leseni pamoja na Serikali kukosa mapato.

## FUNGU H02 HOSPITALI YA MNAZI MMOJA

## PROGRAMU KUU YA HUDUMA ZA UCHUNGUZI NA MATIBABU

**Mheshimiwa Spika,**
Kiujumla utekelezaji wa **Programu Kuu** hii ya **PH0201** hutekelezwa kupitia huduma kuu mbili ikiwemo utoaji wa Huduma za Uchunguzi kwa Wagonjwa pamoja na utoaji wa Huduma za Matibabu kwa Wananchi wote wanaofika katika hospitali zetu ambapo huduma hizi husimamiwa na kutolewa chini ya utekelezaji wa **Programu Ndogo** mbili ambazo **SH020101** na **SH020102** zinazotelezwa kupitia Programu Kuu hii.

**Mheshimiwa Spika,**
Kamati, inaipongeza Serikali kwa kuanzisha utaratibu wa chanzo cha nje (Out Source) kwa huduma za vipimo na uchunguzi katika hospitali zetu zote za Wilaya, Mkoa pamoja na Rufaa kwa ajili ya kuwapatia huduma bora wananchi wake.
**Mheshimiwa Spika,**
Kamati, inapendekeza kwa Serikali kuandaa utaratibu mzuri wa usimamizi na uendeshaji pamoja na udhibiti wa mapato yatokanayo na

huduma hizo
zitakazokuwa zinatolewa na kampuni walizofunga nazo mkataba. Vile vile, kuangalia kampuni hizo zinatoa kipaumbele cha ajira kwa wazawa na wataalamu waliokuwa waajiriwa wa SMZ.

**Mheshimiwa Spika,**
Mwisho kabisa, napenda kuwashukuru kwa dhati Waheshimiwa Wajumbe wa Baraza hili Tukufu kwa umakini na usikivu wao wa hali ya juu wakati wote nilipokuwa nikiwasilisha hotuba hii. Kwa vile Kamati ya Ustawi wa Jamii imepitia, imejadili na kuyakubali mapendekezo ya Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Afya, naomba sasa nichukue fursa hii kuwaomba Waheshimiwa Wajumbe wa Baraza hili kuichangia, kuijadili, kuhoji na hatimaye kuipitisha bajeti ya Wizara ya Afya kwa mwaka wa fedha wa 2023/2024.

**Mheshimiwa Spika,**
Baada ya kusema hayo, Kwa niaba Kamati ya Ustawi wa Jamii pamoja na wananchi wa Jimbo la Konde naiunga mkono hoja kwa asilimia mia moja, na naomba kuwasilisha.

Ahsante sana,

……………………..
**Mhe. Zawadi Amour Nassor,**
**Kny. Mwenyekiti,**
**Kamati ya Ustawi wa Jamii,**
**Baraza la Wawakilishi,**
**Zanzibar.**